

### Taarifa kwa Vyombo vya Habari

#### **Umbile la Kiyahudi Linaanza tena Mauaji Yake**

**Simamisheni tena Khilafah kwa Njia ya Utume kwa ajili ya Uhamasishaji wa Ummah na Majeshi Yake**

**(Imetafsiriwa)**

Umbile la Kiyahudi limeanza tena mauaji yake ya Waislamu wa Gaza. Linajaza angani kwa moshi na moto, huku likiinyweshwa ardhi kwa damu na machozi ya Waislamu. Umbile la Kiyahudi linapigana vita na wanawake na watoto wetu, huku kambi zake za kijeshi zikiwa ndani ya masafa ya makombora ya Pakistan. Umbile la Kiyahudi linamwaga damu safi ya Waislamu, huku askari wa Pakistan wakitumwa kote ulimwenguni, na uongozi wa Pakistan, pamoja na Qatar, ambazo hutoa Laini ya moja kwa moja ya Ardhini ya Mawasiliano kwa Gaza. Umbile la Mayahudi linashambulia huku kukiwa hakuna jeshi la kurudisha mashambulizi yake, hata ingawa Mwenyezi Mungu (swt) ameamrisha,

[وَأَقْتُلُوهُمْ حَيْثُ تَقْتُلُوهُمْ وَأَخْرِجُوهُمْ مِّنْ حَيْثُ أَخْرَجُوكُمْ]

**“Na wauweni popote muwakutapo, na muwatoe popote walipo kutoeni.”** [Surah Al-Baqarah: 191].

Watawala wa Pakistan wanasubiria muda kwa ajili ya umbile la Kiyahudi. Wanawazuia Waislamu na askari wao kutii amri ya Mwenyezi Mungu (swt) kuhusiana na adui anayeshambulia. Watawala hao duni wanatoa udhuru wa umaskini, huku wakifanya kazi na Makruseda kuifukarisha nchi, licha ya kuwa imejaa rasilimali zenye thamani zaidi ulimwenguni. Watawala wadanganyifu wanatoa udhuru wa uadui kati ya Waislamu, huku wao wenyewe wakichochea uadui kwa kueneza mgawanyiko wa kitaifa, badala ya kuamiliiana na Ummah kwa msingi wa Iman, udugu na umoja. Watawala wasaliti wanatoa udhuru kwamba maadui wanaotuzunguka watatushambulia, ingawa wanawafanya Waislamu kuwa madhaifu mbele ya maadui zao, kwa kujisalimisha kwa mfumo wa Kilimwengu wa Kimagharibi, ambao umeuchana mwili wa Ummah wa Kiislamu katika dola zaidi ya hamsini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) aumalize utawala wa watawala hawa wa duni, wadanganyifu na wasaliti hivi karibuni!

**Enyi Waislamu wa Pakistan!** Simameni kuuhami Msikiti wa Al-Aqsa. Vita juu ya Msikiti wa Al-Aqsa, ardhi ya Israa na Miraj ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), vilianza mnamo 1948, sio Oktoba 2023. Tangu wakati huo hadi sasa Hukmu ya Mwenyezi Mungu (swt) ni ile ile, ambayo ni kukabiliana na jeshi la adui, kwa jeshi la waumini. Ama watoto wenu, ndugu na baba zenu walio ndani ya vikosi vya jeshi, wao ni nyinyi na nyinyi wao. Wao hawana utulivu na wana uchungu, kama mulivyo nyinyi. Tofauti kati yao na nyinyi ni kwamba wana utashi, mafunzo na njia za kimada kumaliza sababu ya maumivu hayo, umbile la Kiyahudi. Wakumbusheni kwamba endapi watawapindua watawala hawa na kutaharaki, nyinyi mtawaunga mkono, pamoja na Ummah mzima wa Kiislamu. Na zaidi ya yote Mwenyezi Mungu (swt) huwanusuru waja wake, waumini na watiifu.

**Enyi Waislamu wa Vikosi vya Jeshi la Pakistan!** Utiifu wenu ni kwa Mwenyezi Mungu (swt) juu ya mtu yeyote. Toba kwa madhambi iko katika kujitahidi katika kumtii Mwenyezi Mungu (swt). Hakuna kitendo kikubwa cha utiifu kuliko Jihad. Hakuna ujira mkubwa kuliko ule wa shahidi. Amri ya Mwenyezi Mungu (swt) ni kutaharaki kuwanusuru Waislamu wa Gaza. Hamuwezi kuasi. Uongozi wa Pakistan kamwe hautakutumeni. Umetoa salimisha utashi wake wa kisiasa kwa wakoloni. Muondoeni mtu yeyote anayekuzuieni. Simamisheni uongozi wa kisiasa utakaohamasisha Ummah mzima, na majeshi yake, kuwashinda maadui, na kuwalazimisha kusalimu amri. **Enyi watoto wa Muhammad bin Qasim!** Ni Khilafah kwa Njia ya Utume pekee ndiyo itakayokusaidieni katika harakati za kutafuta shahada na ushindi. Kwa hivyo toeni nusrah yenu kwa Hizb ut Tahrir na mumsage sage adui!

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Pakistan**